# DOYEN PUBLISHERS
## SCHEMES OF WORK TERM II 2025
## GRADE 6 KISWAHILI

| Wk | Lsn | Strand/ Theme | Sub strand | Specific learning outcomes | Key inquiry Questions | Learning experiences | Learning Resources | Assessment methods | Refl |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | **Kuandika** | Barua rasmi | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua barua rasmi kwa kuzingatia muundo wake<br>b) kutambua vipengele vya barua rasmi ili kuvizingatia katika uandishi<br>c) kuchangamkia umuhimu wa barua rasmi katika mawasiliano. | 1. Barua rasmi ni gani?<br>2. Unazingatia nini unapoandika barua rasmi? | Mwanafunzi:<br>• atambue barua rasmi kwenye kielelezo cha barua rasmi iliyochapishwa au kwenye tarakilishi<br>• ashirikiane na wenzake kujadili vipengele vya barua rasmi (*k.v. anwani ya mwandishi [jina, sanduku la posta, tarehe], anwani ya mpokeaji [cheo, sanduku la posta], mtajo, mada ya barua, mwili, hitimisho, sahihi* na *jina la mwandishi)* | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti, kielelezo cha insha<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 45-47<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 54-56 | Maswali na majibu<br>Shajara | |
| | 2 | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya barua rasmi ili kuvizingatia katika uandishi<br>b) kuandika barua rasmi kwa kufuata kanuni zifaazo<br>c) kuchangamkia umuhimu wa barua rasmi katika mawasiliano. | 1. Barua rasmi ni gani?<br>2. Unazingatia nini unapoandika barua rasmi? | Mwanafunzi:<br>• aandike barua rasmi kwa mwalimu akiomba kujiunga na klabu shuleni (*k.v. vile skauti, kilimo na muziki*), akishirikiana na wenzake darasani, kwa hati za mkono au kwa kutumia kifaa cha kidijitali akizingatia muundo wa uandishi wa barua rasmi<br>• aandike barua rasmi katika daftari akiwa peke yake<br>• ajadiliane na wenzake kuhusu | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti, kielelezo cha insha<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 45-47<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 54-56 | Maswali na majibu<br>Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | umuhimu wa barua rasmi katika mawasiliano | | | |
| | **3** | **Sarufi** | Umoja na Wingi wa Nomino: Ngeli ya YA-YA | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za ngeli<br>ya YA-YA katika matini mbalimbali ili kuzibainisha<br>b) kuandika nomino za ngeli ya<br>YA-YA katika umoja na wingi<br>c) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya YA-YA katika mawasiliano. | Je, unajua majina gani ya vitu visivyohesabika? | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya YA-YA kwenye kadi za maneno, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno *(k.m. maji, maziwa, mate, marashi na maskani)*<br>• aandike nomino katika ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 47-48<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 57-59 | Maswali na majibu Shajara | |
| | **4** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kuandika nomino za ngeli ya<br>YA-YA katika umoja na wingi<br>b) kuandika umoja na wingi wa<br>mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya YA-YA<br>c) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya YA-YA katika mawasiliano. | Je, unajua majina gani ya vitu visivyohesabika? | Mwanafunzi:<br>• asikize usomaji wa nomino za<br>ngeli ya YA-YA kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• aandike mafungu ya maneno yenye nomino za ngeli ya YAYA katika umoja na wingi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia nomino za ngeli ya YA-YA kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 47-48<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 57-59 | Maswali na majibu Shajara | |
| **2** | **1** | | Umoja na Wingi wa Sentensi: Ngeli | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze: | Je, unajua majina gani ya vitu ambayo hayabadiliki katika umoja na | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya ngeli ya YAYA katika sentensi kwa kuvipigia mstari au | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | ya YA-YA | a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya YA-YA kwenye sentensi<br>b) kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya nomono za ngeli ya YAYA katika mawasiliano. | wingi? | kuvikoleza rangi katika tarakilishi<br>• atumie nomino za ngeli ya YA-YA katika sentensi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>. | Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 48-49<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 59-60 | | |
| | **2** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya YA-YA kwenye sentensi<br>b) kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya YA-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya nomono za ngeli ya YAYA katika mawasiliano. | Je, unajua majina gani ya vitu ambayo hayabadiliki katika umoja na wingi? | • asikilize usomaji wa sentensi zilizotungwa kutokana na nomino za ngeli ya YA-YA kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• atunge sentensi sahihi kwa kutumia nomino za ngeli ya YA-YA akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wengine<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya YA-YA kwa maandishi ya mkono au tarakilishi | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 48-49<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 59-60 | Maswali na majibu Shajara | |
| | **3** | **Mshika mano wa Kitaifa** | Kusikiliza na kuzungumza | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika matini<br>b) kueleza maana na matumizi ya methali mbalimbali | 1. Je, ni nini umuhimu wa methali katika jamii?<br>2. Ni methali gani unazozijua kuhusu umoja na ushirikiano? | Mwanafunzi:<br>• atambue methali zinazohusu umoja na ushirikiano (*kama vile; umoja ni nguvu utengano ni udhaifu, jifya moja haliinjiki chungu, kidole kimoja hakivunji chawa, kinga na kinga ndio moto huwaka n.k.*) | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 50-52 | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | zinazohusu umoja na ushirikiano katika jamii<br>c) kuchangamkia matumizi ya methali zinazohimiza umoja na ushirikiano. | | katika chati, ubao na vyombo vya kidijitali<br>• atoe mifano ya methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika jamii<br>• asikilize methali za umoja na ushirikiano zikitumiwa kupitia vyombo vya kidijitali | Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 61-64 | | |
| | **4** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana na matumizi ya methali mbalimbali zinazohusu umoja na ushirikiano katika jamii<br>b) kutumia methali zinazohusu umoja na ushirikiano katika mawasiliano<br>c) kuchangamkia matumizi ya methali zinazohimiza umoja na ushirikiano. | 1. Je, ni nini umuhimu wa methali katika jamii?<br>2. Ni methali gani unazozijua kuhusu umoja na ushirikiano? | Mwanafunzi:<br>• ajadili na wenzake maana na matumizi ya methali mbalimbali zinazohusu umoja na ushirikiano<br>• alinganishe methali na maana yake<br>• akamilishe methali mbalimbali zinazohusu umoja na ushirikiano katika mazungumzo akishirikiana na wenzake, kwenye daftari au kwa kutumia vyombo vya kidijitali.<br>• asakure mtandaoni kwa kusaidiwa na mzazi au mlezi wake ili kupata methali zaidi zinazohusu umoja na ushirikiano na matumizi ya methali hizo<br>• ajadili na wenzake kuhusu methali alizozipata mtandaoni ili wajengane kimaarifa. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 50-52<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 61-64 | Maswali na majibu Shajara | |
| **3** | **1** | **Kusoma** | Lugha katika Ushairi | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili dhana za ukwapi na utao katika shairi ili kuzibainisha | Je, kuna tofauti gani kati ya mashairi mbalimbali? | Mwanafunzi:<br>• ashirikiane na wenzake katika vikundi, kujadili ukwapi na utao katika shairi<br>• atambue ukwapi na utao katika shairi kwenye ubao, | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | b) kutambua mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia kwa kuzingatia muundo<br>c) kuchangamkia usomaji wa mashairi ili kuyathamini. | | chati, vitabu au vyombo vya kidijitali<br>• ashirikiane na wenzake kusoma shairi akizingatia ukwapi na utao<br>• ajirekodi akisoma aina za mashairi lengwa akitumia vyombo vya kidijitali ili kuweza kujirekebisha anakokosea<br>• atofautishe mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia kwenye ubao, chati, vitabu au vifaa vya kidijitali | Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 53-54<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 64-67 | | |
| | **2** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia kwa kuzingatia muundo<br>b) kusoma mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia ili kupata ujumbe<br>c) kuchangamkia usomaji wa mashairi ili kuyathamini. | Je, kuna tofauti gani kati ya mashairi mbalimbali? | Mwanafunzi:<br>• atambue mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia katika matini mbalimbali<br>• ashirikiane na wenzake kusoma mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia kwa mahadhi mbalimbali<br>• ashirikiane na wenzake kujadili ujumbe kwenye shairi waliyoyasoma<br>• ajibu maswali yanayotokana na mashairi aliyoyasoma<br>• akisaidiana na mzazi au mlezi, asakure mtandaoni ili kusoma mashairi ya tathnia, tathlitha na tarbia<br>• aandike ujumbe alioupata katika mmojawapo wa mashairi aliyoyasoma na kuwasomea wenzake darasani. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 53-54<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 64-67 | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3 | **Kuandika** | Insha ya maelezo | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha za maelezo katika matini mbalimbali<br>b) keueleza vidokesho katika insha ya maelezo<br>c) kuchangamkia utunzi bora maishani. | Insha ya maelezo ina sifa gani? | Mwanafunzi:<br>• atambue vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• ashiriki na wenzake kujadili vidokezo vya insha ya maelezo atakavyovitumia katika kuandika insha yake<br>. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti, kielelezo cha insha<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 54-56<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 67-70 | Maswali na majibu Shajara | |
| | 4 | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha za maelezo katika matini mbalimbali<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kufuata kanuni zifaazo<br>c) kuchangamkia utunzi bora maishani. | Insha ya maelezo ina sifa gani? | • aonyeshe umilisi wa ubunifu kwa kuandika insha ya maelezo (*k.v. Siku ya sherehe ya kitaifa, Siku ya michezo ya kitaifa, Nchi yetu, n.k*) isiyopungua maneno 200 akizingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na lugha ya kiubunifu inayojumuisha methali na nahau alizojifunza awali ili kutoa picha dhahiri kuhusu anachokielezea<br>• akuze umilisi wa ujuzi wa kidijitali kwa kuandika insha ya maelezo na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti, kielelezo cha insha<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 54-56<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 67-70 | Maswali na majibu Shajara | |
| 4 | 1 | **Sarufi** | Umoja na Wingi wa | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze: | Je, ni nomino zipi hupatikana katika ngeli ya U-U ? | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya U-U (*k.m: uji, ugali,* | chati, tarakilishi vifaa vya | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Nomino: Ngeli ya U-U | a) kutambua nomino katika ngeli ya U-U katika matini mbalimbali ili kuzibainisha<br>b) kuandika nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi<br>c) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya U-U katika mawasiliano. | | *uhuru, ujanja, urafiki*) kwenye kadi za maneno, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• atambue nomino katika ngeli ya U-U katika sentensi<br>• atambue nomino katika ngeli ya U-U katika kifungu kifupi | kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 56-58<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 70-73 | | |
| | **2** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kuandika nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi<br>b) kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya U-U<br>c) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya U-U katika mawasiliano. | Je, ni nomino zipi hupatikana katika ngeli ya U-U ? | Mwanafunzi:<br>• aandike daftarini mwake nomino katika ngeli ya U-U katika umoja na wingi<br>• asikize usomaji wa nomino za ngeli ya U-U kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• aandike mafungu ya maneno yenye nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia nomino za ngeli ya U-U kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 56-58<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 70-73 | Maswali na majibu Shajara | |
| | **3** | | Umoja na Wingi wa Sentensi: Ngeli ya U-U | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-U kwenye sentensi<br>b) kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya U-U | Je, unakumbuka nomino zipi ambazo zinaanza kwa herufi U katika umoja? | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya ngeli ya UU katika sentensi kwa kuvipigia mstari au kuvikoleza rangi katika tarakilishi<br>• atumie nomino za ngeli ya U-U katika sentensi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 59-60 | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya ngeli<br>ya U-U katika mawasiliano. | | . | Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 73-74 | | |
| | **4** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-U<br>kwenye sentensi<br>b) kutunga sentensi akitumia<br>nomino za ngeli ya U-U katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya ngeli<br>ya U-U katika mawasiliano. | Je, unakumbuka nomino zipi ambazo zinaanza kwa herufi U katika umoja? | Mwanafunzi:<br>• asikize usomaji wa sentensi zilizotungwa kutokana na nomino za ngeli ya U-U kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• atunge sentensi kwa kutumia nomino ya ngeli ya U-U akiwa<br>peke yake au kwa kushirikiana na wengine<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya U-U kwa maandishi ya mkono au tarakilishi | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 59-60<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 73-74 | Maswali na majibu<br>Shajara | |
| **5** | **1** | **USAWA WA KIJINSIA** | Kusikiliza na kuzungumza: Matamshi Bora: Ushairi Sauti lengwa:<br>-d/nd<br>-ch/sh<br>-j/nj<br>-g/ng) | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) Kukariri au kuimba shairi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi ya maneno yenye sauti lengwa na mahadhi mbalimbali ili kukuza matamshi bora.<br>b) kueleza maana ya maneno yenye sauti | Kwa nini kusoma na kukariri mashairi ni muhimu? | Mwanafunzi:<br>• asikilize shairi kuhusu suala lengwa na lenye maneno yenye sauti lengwa (**d/nd, ch/sh, j/nj na g/ng**) likikaririwa na mwalimu, mgeni<br>mwalikwa au kifaa cha kidijitali<br>• akariri akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 61-62<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 75-76 | Maswali na majibu<br>Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | lengwa yaliyotumika katika shairi<br>c) kuonyesha ufahamu wa ujumbe katika shairi kwa kujibu maswali kuchangamkia mahadhi mbalimbali katika ushairi. | | shairi kuhusu suala lengwa kwa<br>kuzingatia matamshi ya maneno<br>yenye sauti lengwa na mahadhi<br>mbalimbali<br>• atamke maneno yaliyoundwa<br>kutokana na sauti d/nd, ch/sh, j/nj na g/ng katika shairi<br>• atambue msamiati uliotumika<br>katika ushairi kuhusu usawa wa<br>kijinsia (*k.m. jinsia, ubaguzi, motto wa kiume, mtoto wa kike, usawa, heshima na uwajibikaji*) | | | |
| | **2** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya maneno yenye sauti lengwa yaliyotumika katika shairi<br>b) kutumia kwa usahihi msamiati uliotumiwa katika shairi kuboresha mawasiliano<br>c) kuonyesha ufahamu wa ujumbe katika shairi kwa kujibu maswali kuchangamkia mahadhi mbalimbali katika ushairi. | Kwa nini kusoma na kukariri mashairi ni muhimu? | Mwanafunzi:<br>• atumie msamiati uliotumika katika shairi kutunga sentensi sahihi akiwa peke yake, wawili wawili au katika vikundi<br>• asakure mtandaoni, akishirikiana na wenzake, ili kukariri au kuimba<br>shairi kwa mahadhi mbalimbali<br>• ashirikiane na wenzake kujadili ujumbe katika shairi walililiimba<br>• ajibu maswali yanayotokana na shairi alilosikiliza, aliloimba au kukariri. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 61-62<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 75-76 | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | • aendelee kusoma mashairi katika vitabu na mtandaoni ili kukuza hamu ya ujifunzaji. | | | |
| | **3** | **Kusoma** | Kusoma kwa mapana: Makala | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili mambo ya kuzingatia katika kuchagua makala ya kusoma katika maktaba<br>b) kutambua Makala atakayosoma katika maktaba<br>c) kufurahia kusoma makala mbalimbali ili kujenga ufasaha wa lugha. | 1. Je, kwa nini ni muhimu kuwa na mazoea ya kusoma makala au hadithi?<br>2. Kusoma Makala kuhusu usawa wa kijinsia kuna umuhimu gani? | Mwanafunzi:<br>• aeleze umuhimu wa kusoma kwa mapana<br>• ajadili mambo ya kuzingatia anapochagua matini za kusoma<br>katika maktaba (*k.v. makala yanayoambatana na umri, ukubwa wa maandishi, ujumbe anaotaka kuupata*) | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 62-63<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 76-77 | Maswali na majibu<br>Shajara | |
| | **4** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua Makala atakayosoma katika maktaba<br>b) kusoma Makala mbalimbali ili kupata ujumbe<br>c) kufurahia kusoma makala mbalimbali ili kujenga ufasaha wa lugha. | 1. Je, kwa nini ni muhimu kuwa na mazoea ya kusoma makala au hadithi?<br>2. Kusoma Makala kuhusu usawa wa kijinsia kuna umuhimu gani? | Mwanafunzi:<br>• achague makala mbalimbali kuhusu suala lengwa katika maktaba (makala yaliyochapishwa au katika kifaa cha kidijitali)<br>• asome makala ya aina mbalimbali aliyoyachagua<br>• ajadiliane kwa heshima na wenzake kuhusu ujumbe alioupata katika makala aliyoyasoma atumie kamusi kupata maana za msamiati uliotumika katika makala. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 62-63<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 76-77 | Maswali na majibu<br>Shajara | |
| | **5** | **Kuandika** | Insha za Wasifu | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kimuundo vya insha za wasifu ili kuibainisha | Insha ya wasifu ina sifa gani? | Mwanafunzi:<br>• akuze hamu ya ujifunzaji kwa<br>kutazama nakala za insha ya wasifu kwenye chapa au kwenye tarakilishi | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti, kielelezo cha insha | Maswali na majibu<br>Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | b) kuandika vidoekezo vya insha ya wasifu<br>c) kufurahia uandishi wa insha za wasifu kwa kueleza sifa za mtu, kitu, mnyama au mahali. | | • atambue vipengele muhimu vya kimuundo (*k.v. kichwa, mwili, hitimisho*) katika uandishi wa insha ya wasifu | Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 64-65<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 78-79 | | |
| **6** | **1** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kimuundo vya insha za wasifu ili kuibainisha<br>b) kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia sifa zake<br>c) kufurahia uandishi wa insha za wasifu kwa kueleza sifa za mtu, kitu, mnyama au mahali. | Insha ya wasifu ina sifa gani? | Mwanafunzi:<br>• akuze umilisi wa mawasiliano na ushirikiano kwa kujadili na wenzake kuhusu mada mbalimbali zinazoweza kutungiwa insha za wasifu<br>• Aandike kwenye kitabu chake aukwenye tarakilishi insha ya wasifuisiyopungua maneno 200 kwa kuzingatia msamiati na ujumbe unaohusu suala lengwa. Pia azingatie ujumbe, tahajia, anwani, muundo na mtindo<br>• Awasomee wenzake insha aliyoiandika. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti, kielelezo cha insha<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 64-65<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 78-79 | Maswali na majibu Shajara | |
| **7** | **HALF TERM** | | | | | | | | |
| | **2** | **Sarufi** | Umoja na Wingi wa Nomino: Ngeli ya I-I | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino katika ngeli ya I-I katika matini mbalimbali ili kuzibainisha<br>b) kuandika nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi | Je, ni nomino zipi hupatikana katika ngeli ya I-I ? | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya I-I (*k.v. chumvi, miwani na sukari, chai, kahawa, mirathi, asali, sharubati*)<br>kwenye kadi, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno<br>• atambue nomino katika ngeli ya I-I katika sentensi | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 65-67 | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | c) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya I-I katika mawasiliano. | | • atambue nomino katika ngeli ya I-I katika kifungu kifupi | Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 80-82 | |
| | **3** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kuandika nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi<br>b) kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya I-I<br>c) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya I-I katika mawasiliano. | Je, ni nomino zipi hupatikana katika ngeli ya I-I ? | Mwanafunzi:<br>• aandike nomino katika ngeli ya I-Ikatika umoja na wingi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa nomino za ngeli ya I-I kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• aandike mafungu ya maneno yenye nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia nomino za ngeli ya I-I kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 65-67<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 80-82 | Maswali na majibu Shajara |
| | **4** | | Umoja na Wingi wa Sentensi: Ngeli ya I-I | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya I-I kwenye sentensi<br>b) kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya ngeli ya I-I katika mawasiliano | Je, nomino za ngeli ya I-I huchukua viambishi gani katika sentensi? | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya ngeli ya I-I katika sentensi kwa kuvipigia mstari au kuvikoleza rangi katika tarakilishi<br>• atumie nomino za ngeli ya I-I katika sentensi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 67-69<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 83-84 | Maswali na majibu Shajara |
| **8** | **1** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze: | Je, nomino za ngeli ya I-I huchukua | • asikize usomaji wa sentensi zilizotungwa kutokana na nomino za ngeli ya I-I | chati, tarakilishi vifaa vya | Maswali na majibu Shajara |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya I-I kwenye sentensi<br>b) kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya I-I katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya ngeli ya I-I katika mawasiliano | viambishi gani katika sentensi? | kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• atunge sentensi kwa kutumia nomino ya ngeli ya I-I akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wengine<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya I-I kwa maandishi ya mkono au tarakilishi | kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 67-69<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 83-84 | | |
| | **2** | **MAJANGA NA JINSI YA KUYAZUIA** | Kusikiliza na kuzungumza: Nahau | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nahau za kazi na ushirikiano katika matini mbalimbali<br>b) kujadili maana ya nahau mbalimbali za kazi na ushirikiano ili kuzitofautisha<br>c) kuthamini matumizi ya nahau za kazi na ushirikiano katika mawasiliano. | Je, ni nahau zipi zinazohimiza watu kufanya mambo mbalimbali? | Mwanafunzi:<br>• atambue nahau za kazi na ushirikiano (*k.v. chapa kazi, kunja jamvi, changa bia, sema kwa sauti moja, fanya itifaki*) katika chati, michoro, picha, vikapu maneno, mti maneno, chati, kamusi na katika vyombo vya kidijitali<br>• ashiriki katika kujadili na wenzake maana za nahau za kazi na ushirikiano kwa kutoa mifano | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 70-71<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 85-87 | Maswali na majibu<br>Shajara | |
| | **3** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili maana ya nahau mbalimbali za kazi na ushirikiano ili kuzitofautisha<br>b) kutumia nahau za kazi na ushirikiano katika mawasiliano<br>c) kuthamini matumizi ya nahau za kazi na | Je, ni nahau zipi zinazohimiza watu kufanya mambo mbalimbali? | Mwanafunzi:<br>• aambatanishe nahau na maana yake<br>• atumie nahau za kazi na ushirikiano katika sentensi akiwa pekee au kwa kushirikiana nawenzake<br>• asakure mtandaoni ili kupata nahau zaidi za kazi na ushirikianona maana zake na kuziandika | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 70-71<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha | Maswali na majibu<br>Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ushirikiano katika mawasiliano. | | • awasomee wenzake nahau alizozipata ili kuelimishana | mwanafunzi Uk. 85-87 | | |
| | **4** | **Kusoma** | Kusoma kwa Mapana: Matini | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba<br>b) kuchagua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba<br>c) kufurahia usomaji wa matini za aina mbalimbali ili kujenga utamaduni wa kusoma. | 1. Unapenda kusoma matini ya aina gani?<br>2. Ni vipi unavyoweza kupata matini ya kusoma?<br>3. Kusoma aina mbalimbali za matini kuna umuhimu gani? | Mwanafunzi:<br>• atambue aina mbalimbali za matini (*k.v. vitabu, magazeti, na majarida)* kwenye tarakilishi au kadi za katalogi<br>• ajichagulie matini atakayoisoma<br>• asome matini kimyakimya ili kupata ujumbe uliopo na kufaidi matumizi ya lugha<br>• asimulie ujumbe kutokana na matini alizosoma kwa wenzake<br>• ajadiliane na wenzake matini alizosoma ili kuchochea hamu ya usomaji wa mapana miongoni mwao. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 72-73<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 88-89 | Maswali na majibu<br>Shajara | |
| **9** | **1** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kuchagua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba<br>b) kusoma matini ili kufaidika na ujumbe na lugha inayotumiwa<br>c) kufurahia usomaji wa matini za aina mbalimbali ili kujenga utamaduni wa kusoma. | 1. Unapenda kusoma matini ya aina gani?<br>2. Ni vipi unavyoweza kupata matini ya kusoma?<br>3. Kusoma aina mbalimbali za matini kuna umuhimu gani? | Mwanafunzi:<br>• atambue aina mbalimbali za matini (*k.v. vitabu, magazeti, na majarida)* kwenye tarakilishi au kadi za katalogi<br>• ajichagulie matini atakayoisoma<br>• asome matini kimyakimya ili kupata ujumbe uliopo na kufaidi matumizi ya lugha<br>• asimulie ujumbe kutokana na matini alizosoma kwa wenzake | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 72-73<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 88-89 | Maswali na majibu<br>Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | • ajadiliane na wenzake matini<br>alizosoma ili kuchochea hamu ya usomaji wa mapana miongoni mwao. | | | |
| | **2** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba<br>b) kuchagua matini anazotaka<br>kusoma kwenye maktaba<br>c) kusoma matini ili kufaidika na ujumbe na lugha inayotumiwa<br>d) kufurahia usomaji wa matini<br>za aina mbalimbali ili kujenga<br>utamaduni wa kusoma. | 1. Unapenda kusoma<br>matini ya aina gani?<br>2. Ni vipi unavyoweza kupata<br>matini ya kusoma?<br>3. Kusoma aina mbalimbali<br>za matini kuna<br>umuhimu gani? | Mwanafunzi:<br>• atambue aina mbalimbali za matini (*k.v. vitabu, magazeti, na majarida)* kwenye tarakilishi au kadi za katalogi<br>• ajichagulie matini atakayoisoma<br>• asome matini kimyakimya ili<br>kupata ujumbe uliopo na kufaidi matumizi ya lugha<br>• asimulie ujumbe kutokana na<br>matini alizosoma kwa wenzake<br>• ajadiliane na wenzake matini<br>alizosoma ili kuchochea hamu ya usomaji wa mapana miongoni mwao. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 72-73<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 88-89 | Maswali na majibu<br>Shajara | |
| | **3** | **Kuandika** | Insha ya maelezo | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili maudhui ya insha ya maelezo ili kukuza ubunifu.<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia mada, mtiririko, sarufi, muundo na mtindo ufaao | Unazingatia nini unapoandika insha ya maelezo? | Mwanafunzi:<br>• atambue vifungu vya insha za<br>maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi (*k.v. maelezo kuhusu kuzuia mmomonyoko wa udongo, mafuriko, mitetemeko*<br>*ya ardhi, mkurupuko wa magonjwa kama vile kipindupindu*) | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti, kielelezo cha insha<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 74-75<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha | Maswali na majibu<br>Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | c) kuchangamkia utungaji wa insha za maelezo ili kukuza hali ya kujiamini. | | • ashiriki na wenzake kujadili mada na vidokezo vya insha insha atakayoiandika | mwanafunzi Uk. 89-91 | | |
| | **4** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili maudhui ya insha ya maelezo ili kukuza ubunifu.<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia mada, mtiririko, sarufi, muundo na mtindo ufaao<br>c) kuchangamkia utungaji wa insha za maelezo ili kukuza hali ya kujiamini. | Unazingatia nini unapoandika insha ya maelezo? | Mwanafunzi:<br>• aandike insha ya maelezo isiyopungua maneno 200 akizingatia kategoria za maneno<br>kama vile aina mbalimbali za viwakilishi ifaavyo ili kuuwasilisha ujumbe lengwa, anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu unaojumuisha methali<br>na nahau alizojifunza awali<br>• atunge insha ya maelezo mtandaoni na kuisambaza kwa<br>wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuisoma na kuitathmini | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti, kielelezo cha insha<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 74-75<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 89-91 | Maswali na majibu Shajara | |
| **10** | **1** | **Sarufi** | Umoja na Wingi wa Nomino na Sentensi: Ngeli ya PA-KU-MU | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino katika<br>ngeli ya PA-KU-MU ili kuzibainisha<br>b) kuandika nomino za ngeli<br>ya PA-KU-MU katika umoja na wingi | KUNonimo za ngeli ya PA-KU-MU ni gani? | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya PA-KU-MU kwenye kadi, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno (*k.v: huku, humu, hapa, hapo, huko, humo, pale, kule, mle*)<br>• aandike nomino katika ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na<br>wingi akiwa peke yake, | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 75-77<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | c) kuandika sentensi akitumia nomino za ngeli ya PAKU- MU katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya PAKU- MU katika mawasiliano. | | wawiliwawili au katika kikundi<br>• asikize usomaji wa nomino za ngeli ya PA-KU-MU kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• abadilishe sentensi zenye nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika umoja na wingi<br>• atunge sentensi kwa kutumia nomino ya ngeli ya PA-KU-MU akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wengine<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya PA-KU- MU kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | mwanafunzi Uk. 91-93 | | |
| | 2 | **WANYAMA WA MAJINI** | Kusikiliza na kuzungumza: visawe vya maneno Zaidi ya matatu | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa katika kundi la maneno<br>b) kueleza maana ya kisawe<br>c) kuthamini matumizi ya maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa katika mawasiliano. | Unajua maneno gani ya Kiswahili yaliyo na maana sawa? | Mwanafunzi:<br>• atambue maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa (*k.v. mwiziluja, mkupuzi, pwagu, pwaguzi,mkwepuzi; hongo, rushwa, chai, kadhongo, mvugulio; pesa - njenje, ngwenje, fedha, hela; lengo - dhamira, nia, azma, kusudi; maskini, mlalahoi, fukara, mkata, fakiri)* kwa kutumia kapu lamaneno, kadi za maneno, mti wa maneno, tarakilishi, n.k.<br>• eleze maana ya maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa akiwa peke yake au kwa kujadiliana na | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 78-80<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 94-95 | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | wenzake katika kikundi | | | |
| | 3 | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa katika kundi la maneno<br>b) kutumia visawe ifaavyo katika mawasiliano<br>c) kuthamini matumizi ya maneno zaidi ya matatu yenye maana sawa katika mawasiliano. | Unajua maneno gani ya Kiswahili yaliyo na maana sawa? | Mwanafunzi:<br>• ambatanishe maneno zaidi ya<br>matatu yaliyo na maana sawa katika kapu la maneno, mti wa<br>maneno, ubao, chati, vyombo vya kidijitali, kadi za maneno n.k.<br>• ahusishe visawe na vifaa halisi, picha, michoro kwenye chati, kitabu au katika vyombo vya kidijitali<br>• ashiriki kujadili visawe mbalimbali katika vikundi au wanafunzi wawiliwawili<br>• atumie kisawe kimoja kuchukua nafasi ya kingine katika sentensi. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 78-80<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 94-95 | Maswali na majibu<br>Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4 | **Kusoma** | Kusoma kwa ufahamu: mchezo wa kuigiza | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili sifa za mchezo wa kuigiza ili kuzibainisha<br>b) kusoma mchezo mfupi wa kuigiza kwa ufasaha kwa kuzingatia ujumbe na msamiati wa suala lengwa<br>c) kuonea fahari nafasi ya mchezo wa kuigiza katika jamii. | 1. Je, mchezo wa kuigiza una sifa gani?<br>2. Umewahi kushiriki katika mchezo gani wa kuigiza? | Mwanafunzi:<br>• aeleze maana ya mchezo wa kuigiza akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi<br>• ajadili na wenzake sifa za mchezo wa kuigiza (*k.v. huwa na wahusika, kuna mazungumzo, maelekezo n.k.*)<br>• asome mchezo wa kuigiza akizingatia wahusika, maelekezo na ujumbe | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 80-82<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 96-98 | Maswali na majibu Shajara | |
| **11** | **1** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili sifa za mchezo wa kuigiza ili kuzibainisha<br>b) kusoma mchezo mfupi wa kuigiza kwa ufasaha kwa kuzingatia ujumbe na msamiati wa suala lengwa<br>c) kuonea fahari nafasi ya mchezo wa kuigiza katika jamii. | 1. Je, mchezo wa kuigiza una sifa gani?<br>2. Umewahi kushiriki katika mchezo gani wa kuigiza? | Mwanafunzi:<br>• atambue msamiati wa suala lengwa uliotumiwa katika mchezo wa kuigiza (*k.v. kiboko, samaki, mamba, chura, kasa*)<br>• ashiriki katika majadiliano kuhusu msamiati uliotumiwa katika mchezo wa kuigiza<br>• ajibu maswali kutokana na mchezo aliousoma<br>• atoe muhtasari wa ujumbe ulio katika mchezo wa kuigiza<br>• atazame mchezo mfupi wa kuigiza shuleni au kwenye vifaa vya kidijitali | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 80-82<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 96-98 | Maswali na majibu Shajara | |
| | **2** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kusoma mchezo mfupi wa kuigiza kwa ufasaha kwa kuzingatia ujumbe na | 1. Je, mchezo wa kuigiza una sifa gani?<br>2. Umewahi kushiriki katika mchezo gani wa | Mwanafunzi:<br>• ashiriki mjadala kuhusu ujumbe unaojitokeza kwenye mchezo wa kuigiza<br>• asaidiwe na mzazi au mlezi wake kusakura na kusoma | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | msamiati wa suala lengwa<br>b) kuonyesha ufahamu wa mchezo wa kuigiza kwa kujibu maswali na kutoa muhtasari<br>c) kuonea fahari nafasi ya mchezo wa kuigiza katika jamii. | kuigiza? | mchezo wa kuigiza kwenye mtandao<br>• awaeleze wenzake darasani ujumbe alioupata kutoka kwa mchezo aliousoma mtandaoni. | Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 80-82<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 96-98 | | |
| | **3** | **Kuandika** | Insha za Masimulizi | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili mtiririko wa hoja katika insha ya masimulizi<br>b) kutaja vidokezo katika insha ya mazimulizi<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri katika uandishi wa insha ya masimulizi | Ni nini unachoweza kufanya ili uwe mwandishi bora wa insha? | Mwanafunzi:<br>• ajadili mtiririko wa hoja katika insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• ashiriki na wenzake kujadili muundo wa insha ya masimulizi<br>. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti, kielelezo cha insha<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 82-83<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 98-100 | Maswali na majibu Shajara | |
| | **4** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili mtiririko wa hoja katika insha ya masimulizi<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri katika uandishi wa insha ya masimulizi | Ni nini unachoweza kufanya ili uwe mwandishi bora wa insha? | • aonyeshe ubunifu kwa kuandika insha isiyopungua maneno 200 inayosimulia tukio linalohusiana na wanyama wa porini akizingatia nomino na vivumishi mbalimbali, mnyambuliko wa vitenzi, anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka, lugha ya kiubunifu na urefu unaotarajiwa<br>• akuze ujuzi wa kidijitali kwa kuandika insha ya masimuizi | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti, kielelezo cha insha<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 82-83<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 98-100 | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | katika vifaa vya kidijitali na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili waitathmini na kumwelekeza | | | |
| **12** | **1** | **Sarufi** | Mnyambu liko wa Vitenzi: Kauli ya Kutendean a, Kutendesh a, Kutendua | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika matini<br>b) kutumia vitenzi katika hali za kutendeana, kutendesha, kutendua ipasavyo katika sentensi<br>c) kuchangamkia matumizi ya vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika mawasiliano. | Je, vitenzi vinaweza kubadilika vipi mwishoni ili kuleta maana mbalimbali? | Mwanafunzi:<br>• atambue vitenzi katika hali za<br>kutendeana, kutendesha na kutendua katika chati, jedwali,<br>kapu la maneno, mti wa maneno, ubao na vyombo vya kidijitali | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 84-85<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 100-102 | Maswali na majibu Shajara | |
| | **2** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika matini<br>b) kutumia vitenzi katika hali za kutendeana, kutendesha, kutendua ipasavyo katika sentensi<br>c) kuchangamkia matumizi ya vitenzi katika hali ya kutendeana, | Je, vitenzi vinaweza kubadilika vipi mwishoni ili kuleta maana mbalimbali? | Mwanafunzi:<br>• anyambue vitenzi katika hali lengwa akiwa peke yake, wakiwa wawiliwawili au katika<br>vikundi<br>• atumie vitenzi katika hali lengwa kwenye sentensi | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 84-85<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 100-102 | Maswali na majibu Shajara | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | kutendesha, kutendua katika mawasiliano. | | | | | |
| | **3** | | | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika matini<br>b) kutumia vitenzi katika hali za kutendeana, kutendesha, kutendua ipasavyo katika sentensi<br>c) Kuchangamkia matumizi ya vitenzi katika hali ya kutendeana, kutendesha, kutendua katika mawasiliano. | Je, vitenzi vinaweza kubadilika vipi mwishoni ili kuleta maana mbalimbali? | Mwanafunzi:<br>• atumie vitenzi katika hali lengwa kwenye sentensi<br>• ashirikiane na wenzake kujaza mapengo katika jedwali la mnyambuliko we vitenzi kwenye daftari au kwa kutumia tarakilishi<br>• aandike sentensi upya kwa kutumia vitenzi katika hali mbalimbali. | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 84-85<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 100-102 | Maswali na majibu<br>Shajara | |
| | **4** | **AFYA YA AKILI** | Kusikiliza na kuzungumza: Mazungumzo katika miktadha rasmi na isiyo rasmi | Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua miktadha rasmi na isiyo rasmi katika mawasiliano ili kuitofautisha<br>b) kutaja lugha zinazotumika katika miktadha rasmi.<br>c) Kuchangamkia matumizi ya lugha katika miktadha rasmi na isiyo rasmi kuimarisha maadili yafaayo. | 1. Ni wapi katika shughuli zetu za kila siku tunaitumia lugha rasmi na isiyo rasmi?<br>2. Ni nini kinachofanya mazungumzo yawe rasmi au yasiyo rasmi? | Mwanafunzi:<br>• atambue miktadha mbalimbali kunakotumiwa lugha rasmi na isiyo rasmi *(k.v. ofisini, hospitalini, nyumbani, sokoni)*<br>• asikilize mazungumzo rasmi na yasiyo rasmi kwa kutazama maigizo kwenye vyombo vya kidijitali *(k.v. video, rununu, runinga, tarakilishi)*<br>• ashiriki katika maigizo ya mazungumzo ya miktadha rasmi na yasiyo rasmi akishirikiana na wenzake | chati, tarakilishi vifaa vya kidijitali, simu, tabuleti<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 TG Uk. 86-88<br><br>Kiswahili Sahili Grd 6 kitabu cha mwanafunzi Uk. 103-106 | Maswali na majibu<br>Shajara | |
| **13-14** | **ASSESSMENT AND CLOSING** | | | | | | | | |